# Kanuni ya Maadili

**Mazoea Bora na Thabiti ya Jamii ya Women Deliver na Makubaliano ya Programu ya Viongozi Chipukizi**

Kanuni hizi za Maadili zinatumika kwa wafanyakazi wote wa Women Deliver, washauri, wadau, na washiriki katika Programu ya Viongozi Chipukizi. Kanuni hizi za Maadili zinaongezea, na hazichukui nafasi kwa njia yoyote ile ya **sera zote za Women Deliver** zilizopo, ikiwemo **Sera ya Ulinzi Salama wa Watoto na Vijana**. Kukosa kutii Kanuni hizi za Maadili kunaweza kusababisha hatua za kinidhamu, ikijumuisha kusitishwa kwa kazi au kandarasi, au kuondolewa kwenye Programu ya Viongozi Chipukizi.

Je, umeona au kushuhudia tabia ambayo haiambatani na Kanuni hizi za Maadili, au una mawazo kuhusu jinsi Women Deliver wanaweza kufanya mengi zaidi? Tunakuhimiza utuelezee maoni yako; wasiliana moja kwa moja na mwanachama wa Timu ya Uhusiano wa Vijana au andika baruapepe kwa **safeguarding@womendeliver.org**.

**Chuki haina nafasi hapa:** Tunapinga na hatutakubali ubaguzi wa kikabila, , kijinsia, rangi, ukoloni, utabaka, ubaguzi wa umri, uwezo, chuki dhidi ya LGBTQIA+, chuki dhidi ya uanachama, chuki dhidi ya wageni, ubaguzi wa kidini, kuaibishwa kimwili, uonevu, vitisho au unyanyasaji katika shirika la Women Deliver. Tunahimiza hatua za kibinafsi na za pamoja zinazounda mazingira salama, na jumuishi kwa wote ili kuungana na kushirikiana.

**Kujitolea kwa Haki za Binadamu kwa wote:** Shirika la Women Deliver linatetea na kutafuta kuendeleza haki ya uhuru wa kimwili na upeo kamili wa SRHR kwa wote, bila ubaguzi, unyanyapaa, au vizuizi vya ufikiaji Women Deliver inachukua mtazamo unaozingatia haki za binadamu katika utetezi wake, ambao una maana kwamba utetezi wetu umejikita katika kujitolea kwa ulimwengu wote, kutotenganishwa, na kutogawanyika kwa haki za binadamu kwa ujumla wake kwa watu wote. Haki za Binadamu ni za watu wote, bila kujali utambulisho wao mwingi na unaoingiliana; haki zao za kibinadamu haziwezi kuondolewa kwa kuhiari au kwa nguvu; na haki zote za binadamu zinahusiana na zinategemeana. Kama Watetezi wa Haki za Binadamu ("HRDs") na Watetezi wa Haki za Kibinadamu za Wanawake ("WHRDs"), Women Deliver na watetezi wote wanaohusishwa na Women Deliver wanajitolea kufanya kazi kikamilifu ili kukuza na kulinda haki moja au zaidi za binadamu, na bila kukandamiza kwa njia isiyo ya moja kwa moja haki za wengine (tazama **Azimio la watetezi wa haki za binadamu**). Watetezi wote wanaofanya kazi na Women Deliver lazima wajitolee katika kuendeleza huduma za kina za afya ya ujinsia na uzazi za wasichana na wanawake (**ilivyofafanuliwa hapa**). Watetezi wote wanaofanya kazi na Women Deliver wanakubaliana na kuidhinisha kanuni za msingi za Women Deliver kuhusu uhuru wa kimwili, usawa wa kijinsia na utetezi.

# Kanuni ya Maadili

Mazoea Bora na Thabiti ya Jamii ya Women Deliver na Makubaliano ya Programu ya Viongozi Chipukizi

**Tunatoka na tumelelewa katika asili tofauti, uzoefu, mitazamo, na utambulisho tofauti:** Sisi sote ni matokeo ya tamaduni, kanuni za kijamii na lugha tofauti, na ni muhimu tufahamu haki na mapendeleo yetu. Baadhi ya masuala ambayo wengine huyafanya au kuyasema yanaweza kuonekana kuwa ya kushangaza au yasiyo ya kawaida kwetu, na vinginevyo. Badala ya kuwahukumu wengine kwa kuwa tofauti nasi, heri tujitolee kuelewa, kukubali, na kusherehekea tofauti zetu - ndani yetu na miongoni mwa wengine.

**Mazingira ya kukaribisha:** Women Deliver imejitolea kufanya programu zetu kufikiwa na wengi, kuwa jumuishi, zinapinga ubaguzi wa rangi na kupinga ukoloni. Usisite kutufahamisha ikiwa una wasiwasi wowote au unahitaji mazingatio maalumu ili kukuwezesha kushiriki kikamilifu na kwa usawa na kuendelea kutuwajibisha kwa maadili yetu ya Kuleta Mabadiliko. Pia tunawaalika Viongozi Chipukizi kukagua kindani njia za kuwa na kutenda ambazo wangependa kuzibadilisha wao wenyewe.

**Kila kitu kwa idhini:** Idhini ni makubaliano ya hiari, ya uthibitisho, na ya pande zote ambayo yanawasilishwa kwa njia ya maneno au vitendo. Idhini lazima itolewe bila kushinikizwa, kulazimishwa, au vitisho na inaweza kuondolewa wakati wowote ukitaka. Kuomba idhini kunamaanisha kusikiliza kile ambacho wengine wanatuambia na kuheshimu mipaka ya mtu mwingine katika mahusiano ya kijamii, kitaaluma, na ya kimapenzi/ya karibu. Women Deliver ina sera ya kutokubali unyanyasaji na dhuluma za kijinsia (tazama "**Ahadi ya Women Deliver ya Kuzuia Unyanyasaji na Dhuluma za Kijinsia**" ili upate maelezo zaidi).

**Heshima ni muhimu:** Sote tunapaswa kuwa na uwezo wa kuchangia, kusikilizwa, kutumia uwezo wetu, na kuleta mabadiliko muhimu. Ili hilo lifanyike, kila mtu anahitaji kujisikia salama katika nafsi yake halisi. Tutende kwa heshima na bila kutoa hukumu kwa mtu yeyote.

**Zingatia mahitaji yako:** Tutaunda nafasi ya kujitunza na kujituliza katika programu zetu na kukualika kufanya vivyo hivyo katika utetezi wako. Ni muhimu kuipa afya na ustawi wetu wa kiakili kipaumbele ili tupunguze mfadhaiko na wasiwasi, tuepuke kuchoka sana, na kushiriki kadri tuwezavyo. Tafadhali wasiliana na mfanyakazi wa Women Deliver ikiwa unahitaji usaidizi.